



SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TISA WA MWAKA WA WANAHISA

(Imetolewa tena: Mabadiliko ya Tarehe na Ukumbi wa Mkutano)

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba **Mkutano Mkuu wa Tisa wa Mwaka wa Wanahisa** wa Kampuni ya Soko la Hisa la Dar Es Salaam (Dar Es Salaam Stock Exchange PLC) utakaofanyika **Four Points by Sheraton (New Africa Hotel)**, Dar Es Salaam na pia kwa **njia ya Mtandao wa eAGM Mkutano Platform**, siku ya **Jumanne tarehe 25 Juni 2024** kuanzia saa tatu na nusu asubuhi (9.30 a.m.) kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kupitisha ajenda ya Mkutano;
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Nane wa Mwaka;
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Nane wa Mwaka;
4. Kupokea na kupitisha
 - 4.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa Mwaka uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2023;
 - 4.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya DSE na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2023;
 - 4.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya *Fidelity Fund* na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2023;
5. Kuidhinisha Pendekezo la Malipo ya Gawio kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2023;
6. Kupitisha Malipo ya Wakaguzi wa Nje;
7. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa Mwaka wa Fedha 2024;
8. Kuidhinisha Malipo ya Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024;
9. Kuchagua Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi; na
10. Mengineyo.

Maelezo:

- (i) Wanahisa watakaotaka kushiriki katika Mkutano kwa njia ya mtandao, wanatakiwa kutoa taarifa kwa Mwanasheria wa Kampuni kwa njia ya simu na. +255747536696 au kwa barua pepe kupitia info@dse.co.tz na registrar@csdr.co.tz kuanzia tarehe 19 Juni 2024 ili kupatiwa kiunganishi cha Mkutano huo;
- (ii) Mwanahisa atakaye hudhuria Mkutano kwenye Ukumbi atatakiwa kufika na namba yake ya akaunti ya hisa "CDS Account Number" pamoja na kitambulisho chake.
- (iii) Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanahisa ni taasisi/kampuni, mwakilishi anatakiwa kuwa na fomu za uwakilishi ziwe zimegongwa muhuri wa kampuni. Fomu hizo zifikishwe kwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi katika ofisi za DSE kabla ya saa nane mchana (02:00 p.m.) tarehe 24 Juni 2024.
- (iv) Mwanahisa anaweza kumteua Dalali wa Soko, mmoja wa Wakurugenzi wa DSE (Non-Executive Director), au Msajili wa Hisa (CSD & Registry Co. Ltd) kama mwakilishi. Wanahisa wanahamasishwa kutumia wawakilishi na wanashauriwa kuteua wawakilishi kwa kujaza fomu za uwakilishi.
- (v) Vitabu vyenye taarifa za hesabu kwa mwaka 2023 pamoja na fomu ya mwakilishi vitapatikana katika Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo la Kambarage, Mtaa wa Ufukoni na kwa Madalali wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam kuanzia tarehe 19 Juni 2024.
- (vi) Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa tarehe 21 Juni 2024.

Kwa Agizo la Bodi

Mary Stephen Mniwasa
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu na Katibu wa Bodi
3 Juni 2024